# HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA KIWANDA CHA ALIZETI DUTWA TAREHE 16/12/2021.

**MAHUDHURIO YA WAJUMBE**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. M. L.Shiminji | Mwenyekiti wa Halmashauri | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. J. N. Dage | Diwani M/M/K/Halmashauri | Mjumbe |
| 3. Mhe. J. G. Kibuga | Diwani Kata ya Sapiwi | Mjumbe |
| 4. Mhe. J. D. Nyaena | Diwani Kata ya Banemhi | Mjumbe |
| 5. Mhe. D. M. Mapya | Diwani Kata ya Mwadobana | Mjumbe |
| 6. Mhe. D. M. Kanagana | Diwani Kata ya Ngulyati | Mjumbe |
| 7. Mhe. L. Magembe | Diwani Kata ya Gilya | Mjumbe |
| 8. Mhe. L. G. Mahuma | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 9. Bw. H. M. Mbwana | Mkurugenzi Mtendaji (H/W) | Katibu |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. A. M. Kundo (Mb) | Mbunge wa Jimbo la Bariadi | Kwa taarifa |

**MAHUDHURIO YA WATAALAM**

| | |
|---|---|
| 1. Bw. N. J. Shirima | Katibu Tawala Wilaya |
| 2. Bw. B. P. Mahena | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 3. Eng. W. S. Makala | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji |
| 4. Eng. S. L. Nkobi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 5. Bi. R. A. Shashi | Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 6. Bw. F. M. Luhemeja | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 7. Dr. J. R. Mziba | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 8. Bw. J. M. Balele | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 9. Bw. E. R. Ndoto | Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 10. Bw. H. Sholoło | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 11. Bw. D. M. Mkumbo | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 12. Bi. E. K. Nyeme | Mkuu wa Idara ya Usafi na Uhifadhi wa Mazingira |
| 13. Bw. M. J. Makungu | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 14. Bw. S. T. Masungwa | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 15. Bw. J. J. Nyanguleta | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 16. Bw. E. Ng'wenga | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki |
| 17. Bw. A. C. Nkondola | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 18. Bw. A. J. Mwami | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |

| | |
|---|---|
| 19. Bw. W. R. Mussa | Afisa Tarafa Mhango |
| 20. Bi. I. Nyaulingo | Afisa Tarafa Dutwa |
| 21. Bw. K. M. Senso | Afisa Wanyama Pori |
| 22. Bw. E. S. Dalali | Afisa Biashara |
| 23. Bi. C. M. Budodi | Mratibu wa TASAF |
| 24. Bw. B. A. Beti | Mwandishi wa Vikao |
| 25. Bw. G. M. Suga | Mwandishi wa Vikao |

**AGENDA ZA KIKAO**

Wajumbe walikubaliana kuwa agenda zifuatazo zijadiliwe kwenye kikao hicho,

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia agenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 16/11/2021.
4. Yatokanayo na muhtasari wa kikao cha tarehe 16/11/2021
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi mwezi Novemba, 2021.
6. Taarifa ya uendeshaji wa mgodi wa Halmashauri kuanzia tarehe 01/12/2021 hadi 10/12/2021.
7. 0mbi la kibali cha kufanya tathimini ya shughuli za uendeshaji katika mradi wa kiwanda cha mafuta ya Alizeti Dutwa.
8. Taarifa ya kupokelewa kwa fedha kiasi cha sh. 1,320,000,000.00 ya UVIKO-19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa.
9. Mengineyo.
10. Kuahirisha kikao.

**MUHT. NA. 01/05/12/2021: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5:44 asubuhi.

**MUHT. NA. 02/05/12/2021: KURIDHIA AGENDA.**

Wajumbe walikubaliana kuwa agenda 10 zilizowasilishwa zijadiliwe kwenye kikao hicho.

**MUHT. NA. 03/05/12/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA TAREHE 16/11/2021.**

Muhtasari huo ulisomwa kwa wajumbe na kupokelewa. Uliwekwa saini na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao kilichopita.

**MUHT. NA. 04/05/12/2021: YATOKANAYO NA MUHTASARI WA TAREHE 16/11/2021.**

1. **Wajumbe waliazimia kuwa, Mwenyekiti wa Halmashauri kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji waunde Tume kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya kutopatikana mchango wa nguvu za wananchi jambo linalopelekea kukwama kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Miswaki.**

   Ilifafanuliwa kwamba, azimio hilo halijatekelezwa. Aidha, Ofisi ya Mkurugezi Mtendaji imeamua kuendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Miswaki kwa kiasi cha fedha kilichopo.

   Wajumbe walikubaliana na ufafanuzi uliotolewa.

2. **Wajumbe waliazimia kuwa, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ifanye mawasiliano na Ofisi ya Meneja wa TARURA wawahimize Wakandarasi waliopewa kazi/zabuni za ujenzi wa barabara kwenye maeneo ya Halmashauri ili waweze kutekeleza kazi hizo kwa wakati.**

   Ilifafanuliwa kuwa, Barua yenye Kumb. Na. DA.101/317/01D/18 ya tarehe 30/11/2021 imeandikwa kwa Meneja wa TARURA (W) kumtaka kuhakikisha Wakandarasi waliopewa kazi/zabuni za ujenzi wa barabara zilizo kwenye maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi wanamaliza kazi zao kwa haraka na kwa muda uliopangwa ili kuwarahisisishia wananchi kupata huduma.

   Wajumbe walikubaliana na utekelezaji huo na kushauri kuendelea kufanyika kwa ufuatiliaji wa barua hiyo.

3. **Wajumbe waliazimia kuwa, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ifanye mawasiliano na Ofisi ya Meneja wa RUWASA ili kuwakumbusha kutekeleza ahadi ya kusambaza maji ndani ya Kata ya Ngulyati hasa kwenye maeneo ya Taasisi za umma.**

   Ilifafanuliwa kuwa, Barua yenye Kumb. Na. DA.101/317/01D/19 ya tarehe 30/11/2021 imeandikwa kwa Meneja wa RUWASA (W) kumkumbusha kutekeleza ahadi ya kusambaza maji ndani ya Kata ya Ngulyati hasa kwenye maeneo yenye Taasisi za Umma.

   Wajumbe walikubaliana na utekelezaji huo na kushauri kuendelea kufanyika kwa ufuatiliaji wa barua hiyo.

**MUHT. NA. 05/02/12/2021: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI NOVEMBA, 2021.**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kwamba, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya Bariadi ilijiwekea lengo la kupokea na kukusanya kiasi cha Tshs. **31,576,282,411.36**. Kwa kipindi cha mwezi Novemba, 2021, Halmashauri imepokea na kukusanya jumla ya Tshs. **2,329,366,450.68** na mapato ya mwezi Julai–Novemba, 2021 ni Tshs. **12,906,684,723.96** sawa na asilimia **40.87** ya Bajeti ya mwaka 2021/2022.

Aidha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri imekisia kutumia Tshs. **31,576,282,411.36**. Kwa kipindi cha mwezi Novemba, 2021, Halmashauri imetumia Tshs. **2,441,289,013.91** na Matumizi yote Julai-Novemba, 2021 ni Tsh. **9,996,373,776.34** sawa na asilimia **31.66** ya Bajeti ya mwaka 2021/2022.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili taarifa hiyo wajumbe walishauri kutiliwa mkazo kwenye ukusanyaji wa vyanzo vya ushuru wa Mkonge na Nyumba za kulala wageni. Aidha, vyanzo vya Ada ya Usafi wa Mazingira na Ada ya Mazao ya Misitu vitengenezewe mikakati mahsusi ili viweze kukusanywa na kuchangia kwenye mapato ya Halmashauri.

**MUHT. NA. 06/05/12/2021: TAARIFA YA UENDESHAJI WA MGODI WA HALMASHAURI KUANZIA TAREHE 01/12/2021 HADI 10/12/2021.**

Mkuu wa Idara ya Fedha kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kuwa, tarehe 01/12/2021 Ofisi ya Madini Mkoa wa Simiyu ilikabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi leseni ya uchimbaji wa eneo lenye ukubwa upana M 170 na urefu M 280. Ambapo eneo hilo linapakana na leseni zingine 2 za Gideon & Partiners kwa upande wa Magharibi na upande wa kusini linapakana na mgodi wa Pamphili & Partiners.

Halmashauri ilianza kusimamia uzalishaji tarehe 02/12/2021 mara tu baada ya kuonyeshwa mipaka na Ofisi ya Madini Mkoa. Ambapo jumla ya Duara 19 zimeanza uzalishaji huku Duara 47 ziko hatua ya utafiti. Aidha, hadi kufikia tarehe 10/12/2021 jumla ya migao minne imekwishafanyika na jumla ya fedha Sh. 27,071,360.00 imekusanywa kutokana na mauzo ya mifuko 285 ambayo ndio mgao wa Halmashauri.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili walikubaliana nayo.

**MUHT. NA. 07/05/12/2021: OMBI LA KIBALI CHA KUFANYA TATHIMINI YA SHUGHULI ZA UENDESHAJI KATIKA MRADI WA KIWANDA CHA MAFUTA YA ALIZETI DUTWA.**

Mkuu wa Idara ya Mipango kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi inamiliki kiwanda cha kuchakata alizeti tangu mwaka 2019, uendeshaji wa shughuli za kiwanda hicho husimamiwa na Watumishi wa Halmashauri.

Kutokana na majukumu mengine waliyonayo watumishi wanaosimamia kiwanda hicho, imepelekea kazi za kiwanda kutofanyika kwa ufanisi. Hivyo Menejimenti imeomba kufanyika tathimini ya uzalishaji wa kiwanda tangu kilipoanzishwa. Baada ya kupatikana taarifa ya tathimini Halmashauri itaingia mkataba wa ubia na mwekezaji atakayepatikana.

Mkataba huo utaainisha kazi/shughuli pamoja na mgawanyo wa faida kwa Halmashauri na Mbia wakati wa uendeshaji wa kiwanda. Aidha, ikiwa mpango huo utapata ridhaa ya kutekelezwa utaingizwa katika mapitio ya bajeti ya mwaka 2021/2022 Desemba 30, 2021.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili walikubaliana na ombi hilo na kuidhinisha kutumika kwa fedha Sh. 3,500,000.00 kwa ajili ya kuwezesha kufanyika kwa tathimini ya shughuli za uendeshaji katika mradi wa kiwanda cha mafuta ya Alizeti Dutwa.

**MUHT. NA. 08/05/12/2021: TAARIFA YA KUPOKELEWA KWA FEDHA KIASI CHA SH. 1,320,000,000.00 YA UVIKO-19 KWA AJILI YA UJENZI WA MADARASA.**

Mkuu wa Idara ya Mipango kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kuwa, Halmashauri imepokea fedha za Mradi wa kuchochea uchumi na mapambano dhidi ya UVIKO-19 kiasi cha Sh. 1,320,000,000.00 kwa ajili ya Sekta ya Elimu ambapo kitatumika kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya vyumba vya madarasa 44 katika shule za sekondari kwa gharama ya Sh. 880,000,000.00 na madarasa 22 katika shule za msingi shikizi kwa gharama ya Sh. 440,000,000.00. Aidha, ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa utatekelezwa kwa kutumia mtindo wa 'force account'.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili wajumbe walisisitiza kuzingatiwa kwa miongozo iliyotolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19

**MUHT. NA. 09/05/12/2021: MENGINEYO.**

I. Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya kusajiliwa kwa shule shikizi 10.

**MUHT. NA. 08/04/11/2021: KUAHIRISHA KIKAO.**

Mwenyekiti kabla ya kuahirisha kikao alisisitiza kutekelezwa kwa wakati maazimio yote yaliyofikiwa kwenye kikao hicho. Aidha, aliwashukuru wajumbe kwa namna walivyoshiriki kuchangia mijadala wakati wa uwasilishaji na majadiliano ya agenda za kikao hicho. Mwisho aliahirisha kikao saa 10:09 alasiri.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

LEO TAREHE 16/.02/ 2022

| | |
|---|---|
| JINA HALIDI M. MBWANA | JINA MAYALA L. SHIMINJI |
| SAINI [signature] | SAINI [signature] |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| MKURUGENZI MTENDAJI<br>HALMASHAURI YA WILAYA BARIADI | MWENYEKITI<br>HALMASHAURI YA WILAYA<br>BARIADI |

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI DUTWA TAREHE 15/03/2022.

**MAHUDHURIO YA WAJUMBE**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. M. L.Shiminji | Mwenyekiti wa Halmashauri | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. J. N. Dage | Diwani M/M/K/Halmashauri | Mjumbe |
| 3. Mhe. J. G. Kibuga | Diwani Kata ya Sapiwi | Mjumbe |
| 4. Mhe. J. D. Nyaena | Diwani Kata ya Banemhi | Mjumbe |
| 5. Mhe. D. M. Mapya | Diwani Kata ya Mwadobana | Mjumbe |
| 6. Mhe. M. N. Kanagana | Diwani Kata ya Ngulyati | Mjumbe |
| 7. Mhe. L. Magembe | Diwani Kata ya Gilya | Mjumbe |
| 8. Mhe. L. G. Mahuma | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 9. Bw. H. M. Mbwana | Mkurugenzi Mtendaji (H/W) | Katibu |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. A. M. Kundo (Mb) | Mbunge wa Jimbo la Bariadi | Kwa taarifa |

**MAHUDHURIO YA WATAALAM**

| | |
|---|---|
| 1. Bi. S. A. Hamisi | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 2. Bw. M. F Sabaya | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 3. Bw. G. J. Mwaja | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji |
| 4. Eng. S. L. Nkobi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 5. Bi. R. A. Shashi | Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 6. Bw. F. M. Luhemeja | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 7. Dr. J. R. Mziba | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 8. Bw. J. M. Balele | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 9. CPA. G. S. Lwiza | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 10. Bw. H. Shololo | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 11. Bw. D. M. Mkumbo | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 12. Bi. E. K. Nyeme | Mkuu wa Idara ya Usafi na Uhifadhi wa Mazingira |
| 13. Bi. I. A. Bampenja | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 14. Bw. S. T. Masungwa | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 15. Bw. E. Ng'wenga | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki |
| 16. Bw. A. J. Mwami | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 17. Bw. W. R. Mussa | Afisa Tarafa Mhango |

18. Bi. I. Nyaulingo — Afisa Tarafa Dutwa
19. Bw. B. I. Benjamini — Afisa Tarafa Nkololo
20. Bw. D. A. Shirima — Afisa Maliasili Pori
21. Bw. D. J. Ndolenge — Afisa Biashara
22. Bi. C. M. Budodi — Mratibu wa TASAF
23. Bw. G. M. Suga — Mwandishi wa Vikao
24. Bw. B. A. Beti — Mwandishi wa Vikao

**WATAALAM WASIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bw. N. J. Shirima | Katibu Tawala Wilaya | Kwa taarifa |
| 2. Bw. J. J. Nyanguleta | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi | Kwa taarifa |
| 3. Adv. R. M. Cosmas | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria | Kwa taarifa |

**AGENDA ZA KIKAO**

Wajumbe walikubaliana kuwa agenda zifuatazo zijadiliwe kwenye kikao hicho,

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia agenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 16/02/2022.
4. Yatokanayo na muhtasari wa kikao cha tarehe 16/02/2022.
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi mwezi Januari, 2021.
6. Taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo.
7. Taarifa ya miradi ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.
8. Taarifa ya vikundi vilivyopangiwa kupatiwa mkopo kutoka mfuko wa asilimia kumi za Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.
9. Taarifa ya zoezi la utoaji wa chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na kondoo.
10. Mengineyo.
11. Kuahirisha kikao.

**MUHT. NA. 01/08/03/2022: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5:55 asubuhi.

**MUHT. NA. 02/08/03/2022: KURIDHIA AGENDA.**

Wajumbe walikubaliana kuwa agenda 11 zilizowasilishwa zijadiliwe kwenye kikao hicho.

**MUHT. NA. 03/08/03/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA TAREHE 16/02/2022.**

Muhtasari huo ulisomwa kwa wajumbe na kupokelewa. Uliwekwa saini na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao kilichopita.

**MUHT. NA. 04/08/03/2022: YATOKANAYO NA MUHTASARI WA TAREHE 16/02/2022.**

1. **Wajumbe waliazimia kuwa, mapendekezo ya Mkaguzi wa Ndani aliyoyatoa wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa Zahanati 3 za Ikungulyandili, Kilabela na Salaliya yatekelezwe.**

   Ilifafanuliwa kuwa, mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi wa Ndani wakati wa Ukaguzi wa mradi wa ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati 3 za Ikukungulyandili, Kilabela na Salalia yametekelezwa.

   Wajumbe walikubaliana na utekelezaji huo.

2. **Wajumbe waliazimia kuwa, Hoja ambazo hazijafungwa zijibiwe ili ziweze kufungwa kabla au ifikapo kwenye kikao kijacho cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango**

   Azimio halijatekelezwa. Hata hivyo ili kuboresha utekelezaji wa azimio hilo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ameunda Timu ya watu 4 kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa majibu ya hoja hizo, na taarifa ya kazi hiyo itawasilishwa kwenye kikao cha robo ya tatu.

   Wajumbe walisisitiza kuwasilishwa kwa taarifa hiyo kwenye kikao cha robo ya tatu.

3. **Wajumbe waliazimia kuwa, wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wafanye ziara ya mafunzo kwenye Hifadhi ya Serengeti ili kujua changamoto zinazosababisha Hotel zilizomo kwenye Hifadhi kutolipa mapato ya Halmashauri.**

   Azimio limezingatiwa. Ziara ya Kamai ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa ajili ya mafunzo kwenye Hifadhi ya Serengeti ili kujua changamoto zinazosababisha Hotel zilizomo kwenye Hifadhi kutolipa mapato ya Halmashauri imepangwa kufanyika tarehe 25-26/03/2022.

   Wajumbe walikubaliana na utekelezaji huo.

4. **Wajumbe waliazimia kuwa, zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo kwa kuvalisha Hereni, iliagizwa kwamba, idadi ya mifugo ibainishwe na kuelezwa kwa kina namna Halmashauri itakavyonufaika na zoezi hilo.**

Azimio limetekelezwa. Taarifa ya namna Halmashauri itakavyonufaika katika zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo kwa kuvalisha Hereni iliwasilishwa kwa wajumbe na kupokelewa.

Wajumbe walikubaliana na utekelezaji huo.

5. **Wajumbe waliazimia kuwa, kwenye mradi wa ujenzi wa vyumba viwili na ofisi katika shule ya msingi Chungu kazi ya uwekaji wa Sakafu kwenye veranda irudiwe.**

   Azimio limezingatiwa. Kazi ya ukarabati wa sakafu kwenye jengo la madarasa 2 na ofisi 1 kwenye shule ya msingi Chungu imeanza na inatarajia kukamilika mwanzoni mwa mwezi Aprili, 2022.

   Wajumbe walikubaliana na ufafanuzi uliotekelezwa.

6. **Wajumbe waliazimia kuwa, Kokoto zote zisizo na ubora zisipokelewe wala kutumika kwenye mradi wa ujenzi wa shule mpya ya sekondari Gibishi.**

   Azimio limezingatiwa. Usimamizi wa karibu unaendelea kwenye mradi wa ujenzi wa shule mpya ya sekondari Gibishi ili kuhakikisha madini ya ujenzi (kokoto) zizazotumika zinakuwa na kiwango kinachohitajika.

   Wajumbe walikubaliana na uekelezaji huo.

7. **Wajumbe waliazimia kuwa, kasi ya ujenzi kwenye kituo cha afya Matongo pamoja na idadi ya mafundi kwenye mradi huo iongezwe.**

   Azimio limetekelezwa. Kasi ya ujenzi kwenye kituo cha afya Matongo pamoja na idadi ya mafundi ujenzi imeongezwa.

   Wajumbe walikubaliana na utekelezaji huo.

8. **Wajumbe waliazimia kuwa, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri iandike barua ya kumpongeza Meneja wa kiwanda cha Alliance Ginners Limited kwa kufadhili ujenzi wa Zahanati ya Nyamisagusa.**

   Azimio limetekelezwa. Barua yenye Kumb. Na. DE. 101/475/62/27 ya tarehe 09/03/2022 imeandikwa kwa Meneja wa kiwanda cha Alliance Ginners Limited kumpongeza kwa ufadhili wake kwenye ujenzi wa Zahanati ya Nyamisagusa.

   Wajumbe walikubaliana na utekelezaji huo.

9. **Wajumbe waliazimia kuwa, Halmashauri ya Kijiji cha Nyamisagusa iendelee na ujenzi wa miundombinu mingine kwenye Zahanati ya Nyamisagusa ili kuunga mkono juhudi za Mfadhili.**

   Azimio limetekelezwa. Barua yenye Kumb. Na. DE.101/475/62/28 ya tarehe 07/03/2022 imeandikwa kwa Mtendaji wa Kijiji cha Nyamisagusa kumtaka kuhimiza wananchi kuendelea na ujenzi wa miundombinu iliosalia kwenye mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Nyamisagusa.

   Wajumbe walikubaliana na utekelezaji huo.

10. **Wajumbe waliazimia kuwa, Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ifanye ziara ya kutembelea vyanzo vya mapato kwenye migodi iliyopo Bulumbaka, Halawa, Lubaga na Nyawa.**

    Azimio limezingatiwa. Ziara ya kutembelea vyanzo vya mapato kwenye migodi imepangwa kufanyika tarehe 25-26/03/2022.

    Wajumbe walikubaliana na ufafanuzi huo.

11. **Wajumbe waliazimia kuwa, Meneja wa TARURA aalikwe kuhudhuria kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani robo ya pili 2022.**

    Azimio halijatekelezwa. Meneja wa TARURA alialikwa kuhudhuria kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani lakini alishindwa kuhudhuria kwasababu ya udhuru. Aidha, ataalikwa tena kuhudhuria kwenye Mkutano wa robo ya tatu 2021/2022.

    Wajumbe walikubaliana na ufafanuzi huo.

**MUHT. NA. 05/08/03/2022: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI JANUARI, 2022.**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara kwa niaba ya Mkurugenzi Mendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kwamba, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya Bariadi ilijiwekea lengo la kupokea na kukusanya kiasi cha Sh. **31,576,282,411.36**. Kwa kipindi cha mwezi Januari, 2022, Halmashauri imepokea na kukusanya jumla ya Sh. **1,763,122,762.13** na mapato ya mwezi Julai, 2021 hadi Januari, 2022 ni Sh. **17,378,795,300.53** sawa na asilimia **55.043%** ya Bajeti ya mwaka 2021/2022.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri imekisia kutumia Sh. **31,576,282,411.36**. Kwa kipindi cha mwezi Januari, 2022, Halmashauri imetumia Sh. **1,996,519,145.82** na jumla ya Matumizi yote Julai, 2021 hadi Januari, 2022 ni Sh. **15,888,911,892.48** sawa na asilimia **50.32%** ya Bajeti ya mwaka 2021/2022.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili taarifa hiyo walishauri kwamba, vyanzo vya mapato ambavyo makusanyo yake yapo chini ya asilimia 50% vitiliwe mkazo katika ukusanyaji kwenye kipindi kilichobakia kumaliza mwaka wa fedha 2021/2022.

**MUHT. NA. 06/08/03/2022: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO.**

Mkuu wa Idara ya Mipango kwa niaba ya Mkurugenzi Mendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi imepokea kiasi cha Sh. 2,279,855,731.51 kutoka Serikali Kuu mwezi Februari, 2022 ikiwa ni fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2021/2022 fedha hizi zitatekeleza Miradi kwa mchanganuo ufuatao;-

a) Ujenzi wa Jengo la Halmashauri Sh. 1,000,000,000.00
b) Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya majengo ya Upasuaji, Kuhifadhia maiti na Wodi 2 (Wanawake na Wanaume) Sh. 800,000,000.00
c) Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 9 kwa shule za msingi Ikinabushu vyumba 2, Mwagabate vyumba 2, Songambele vyumba 2, Nyamswa chumba 1 na Dilanda vyumba 2 kwa Sh. 112,500,000.00
d) Ukamilishaji wa vyumba 5 vya Maabara za Sekondari za Masewa, Mwadobana, Kasoli, Itubukilo na Ikungulyabashashi kwa Sh. 150,000,000.00
e) Ukamilishaji wa Zahanati 2 za Gilya na Nkindwabiye Sh. 100,000,000.00
f) Elimu bila malipo Sekondari Sh. 30,521,225.50
g) Elimu bila malipo Msingi Sh. 74,375,945.93
h) Shughuli za kuchochea uchumi na mapambano dhidi ya UVIKO-19 Sh. 3,458,560.00

Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili wajumbe walishauri kuongezwa kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za miradi ili zuumike kwa mujibu wa miongozo iliyopo na thamani ya miradi hiyo ilingane na fedha iliyotolewa.

**MUHT. NA. 07/08/03/2022: TAARIFA YA MIRADI YA UJENZI WA MAJENGO YA HOSPITALI YA WILAYA NA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI.**

Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi imepata fedha za miradi ya ujenzi kuoka

Serikali Kuu jumla ya Sh. 1,390,000,000.00 ambayo tayari imeshafanyiwa kazi ya kuwapaa mafundi ujenzi, miradi hiyo ni kama ifuaavyo;-

1) Jengo la watumishi wa afya (staff house 3 in 1) lenye thamani ya Sh. 90,000,000.00 na fundi ujenzi aliyeshinda kazi ya ujenzi wa jengo hilo ni Ezekiel Chombo kwa gharama ya Sh. 13,500,000.00 kazi imeanza mradi upo hatua ya msingi.
2) Jengo la dharura (emergence Medical Department) lenye thamani ya Sh. 300,000,000.00 na fundi ujenzi aliyeshinda kazi ya ujenzi wa jengo hilo ni Reuben Lutonja Matondo kwa gharama ya Sh. 49,000,000.00 kazi imeanza mradi hupo hatua ya umwagaji zege kwenye msingi.
3) Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri awamu ya pili ya ujenzi limepata fedha kiasi cha Sh. 1,000,000,000.00 fundi ujenzi aliyeshinda kazi hiyo ya ujenzi ni Fikiri M. Mnyenyelwa kwa gharama ya Sh. 179,233,500.00

Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili walikubaliana nayo.

**MUHT. NA. 08/08/03/2022: TAARIFA YA VIKUNDI VILIVYOPANGIWA KUPATIWA MKOPO KUTOKA MFUKO WA ASILIMIA KUMI ZA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.**

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa niaba ya Mkurugenzi Mendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ilifanya ufuatiliaji na uhakiki wa miradi ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Walemavu vilivyoomba mikopo kupitia mfuko wa Wanawake, Vijana na Walemavu ambao ni mchango wa alimia 10% ya makusanyo ya ndani.

Uhakiki huo wa vikundi ulifanyika kuanzia arehe 21/01/2022 hadi tarehe 28/01/2022 katika Kata 15 za Kasoli, Kilalo, Itubukilo, Mwasubuya, Sakwe, Sapiwi, Masewa, Banemhi, Mwaumatondo, Nkindwabiye, Nkololo, Mwaubingi, Gibishi, Gilya na Dutwa. Jumla ya vikundi 53 vilihakikiwa kama vimekidhi vigezo na masharti ya kupewa mikopo kupitia fedha za Mfuko wa Wanawake, Vijana na Walemavu asilimia 10% ya makusanyo ya ndani.

Aidha, baada ya uhakiki huo, Kamati ya Mikopo ya Halmashauri ilipitia na kuidhinisha vikundi 25 kupaiwa mkopo wenye thamani ya Sh. 117,500,000.00 kwa mchanganuo wa fedha kiasi cha Sh. 66,000,000.00 (mapato ya ndani) na kiasi cha Sh. 51,500,000.00 (fedha zitokanazo na marejesho ya mikopo).

Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili walikubaliana nayo.

**MUHT. NA. 10/08/03/2022: TAARIFA YA ZOEZI LA UTOAJI WA CHANJO YA SOTOKA YA MBUZI NA KONDOO.**

Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Mkurugenzi Mendaji wa Halmashauri aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe. Alifafanua kuwa, kutokana na matatizo ya vifo vya mbuzi na kondoo hasa kwa mwezi April hadi Juni. Halmashauri ilipeleka taarifa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambapo iliamua kufanya utafiti juu ya mifugo husika. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha uwepo wa ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo. Baada ya matokeo hayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) wametoa chanjo ya kutosha kuchanja Mbuzi na Kondoo 167,000.

Aidha, zoezi la chanjo ya Sotoka kwa Mbuzi na Kondoo litaendeshwa kuanzia mwezi Machi, 2022 na litafanyika kwa siku 20 (siku 5 uhamasishaji na siku 15 uendeshaji wa zoezi). Pia gharama ya chanjo kwa mfugo itakuwa Sh. 350 ambapo kiasi cha Sh. 120 kitatumika kuenesha zoezi na Sh. 230 itaingia kwenye mfuko wa Halmashauri kwa kukatiwa stakabadhi za mashine ya POS baada ya kutolewa fedha ya kazi
Wajumbe walipokea taarifa hiyo. Baada ya kuijadili walikubaliana nayo.

**MUHT. NA. 10/08/03/2022: MENGINEYO.**

1. Kuhusu hoja ya kuwepo kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwadobana ambaye alitekeleza na kukamilisha mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa kwa fedha za UVIKO-19 kiasi cha Sh. 40,000,000.00 na kubaki anadaiwa na wazabuni na mafundi walioshiriki kutekeleza mradi huo. Wajumbe waliazimia kuwa, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ichukue hatua kwa mwalimu huyo.

**MUHT. NA. 11/08/03/2022: KUAHIRISHA KIKAO.**

Mwenyekiti kabla ya kuahirisha kikao alisisitiza kutekelezwa kwa wakati maazimio yote yaliyofikiwa kwenye kikao hicho. Mwisho aliahirisha kikao saa 9:01 alasiri.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

LEO TAREHE 16/02/2022

| | |
|---|---|
| JINA HALIDI .M. MBWANA | JINA MAYALA L. SHIMINGI |
| SAINI [signature] | SAINI [signature] |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA BARIADI | MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA BARIADI |